# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**KARATASI YA 1**

**INSHA**

**Mwongozo wa kusahihisha**

**1. RIPOTI**

- Mtahiniwa atimize maneno 400.
- Hii ni insha ya utunzi wa kiuamilifu kwa hivyo sura ya ripoti iwepo, yaani hii ni insha isiyofululiza bali ina vijichwa.

i. Mpangilio wake.

1. Kichwa.
2. Utangulizi.
3. Ndani ya utangulizi ataje waliohojiwa.
4. Ataje tarehe ya uwasilishaji.
5. Ataje mambo mengine muhimu yaliyofanyika.

ii. Matokeo ya udadisi .

-Ayashughulikie na kuonyesha yale mambo yanayosababisha udanganyifu kwa mfano:
-Wanafunzi kutojitayarisha
-Walimu wakuu wa shule kuhusika ili shule zao zipapate nafasi bora ya kujijengea jina lao na la shule yao.
-Wasimamizi wa mitihani kuzembea kazini.
-Wasimamizi wa mitihani kuhongwa/ufisadi.
-Mitihani ya taifa kuwa migumu.
-Nafasi chache za vyuo vikuu kusababisha wanafunzi kuwa na ushindani mkubwa kiasi cha wengine kutumia hila hii.
-Ukosefu wamaadili mema kwa upande wa wanafunzi.
-Ukosefu wa ulinzi wa kutosha.
-Ukosefu wa mpangilio bora darasani/ukumbini wakati mitihani inapofanywa.
-Ukosefu wa sera madhubuti kuhusu mitihani.
-Walimu wa masomo kuhusika/kujihusisha na udanganyifu ili masomo yao yawe bora zaidi.
-Watahiniwa kusingiziwa tu labda kutokana na historia ya hapo awali.
-Watahini kukosa umakini wa kutambua vyema kama mtihani uliibwa au la.[Hoja zingine zozote]

iii. Mapendekezo.

-Wasimamizi mihahani wawe watu wenye maadili na kujiheshimu.
-Watahiniwa watayarishwe mapema na vya kutosha.
-Sheria madhubuti kubuniwa kudhibiti wizi wa mitihani.
-Vyuo vikuu viongezwe maradufu.
-Mtindo kuorodhesha shule bora katika kaunti na taifa uondolewe.
-Ulinzi uimarishwe.
-Nafasi za kazi zibuniwe kupunguza ushindani mkali uliopo.
-Mtihani uwe wastani/kadri na si mgumu sana.
-Somo la dini liimarishwe ili kuleta maadili miongoni mwa wanafunzi.
-Wasimamizi wa mitihani walipwe vizuri kuzuia kuhongwa.

iv. Hitimisho.

-Mtahiniwa atoe maoni, kauli, msimamo mradi yahusiane na mada husika.
- Insha ikikosa sura ifaayo akaadiriwe ifaavyo kasha aoondolewe alama 4 za sura.

2. Wananchi ndio wa kulaumiwa kufuatana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili.

**Kuunga**

- Chuki na uhasama baina ya makabila/ vita vya kikabila.
- Uundaji wa vikundi haramu vya vijana.
- Tamaa ya kutajirika k.m. wizi wa mifugo.
- Wachochole kuingilia uhalifu kwa madai ya kujitafutia.
- Wananchi kukataa kufichua wahalifu miongoni mwao/ wnawaficha.
- Umiliki wa silaha hatari na baadhi ya wananchi.
- Mitazamo hasi ya wananchi kuhusu maafisa wa usalama/ hawashirikiani nao.

**Kupinga.**

-Usalama unakoseshwa na kutokuwepo kwa nafasi za kazi/ wasio na kazi hulazimika kuingilia uhalifu ili wapate ajira.
-Ukosefu wa fedha za kuendeleza uimarishaji wa usalama.
-Idadi ndogo ya maafisa wa usalama.
-Ufisadi wa maafisa wa usalama.
-Vifaa vya kuendeleza shughuli za usalama k.m. magari, silaha havitoshi.
-Kiwango cha chini cha mafunzo kwa walinda usalama.
-Magaidi wanaotatiza usalama nchini kutoka nchi za kigeni k.v. Somalia ambao huwalemea wananchi.

i. Mtahiniwa asiwe na hoja chini ya tano. Aliye na tatu tu asipite kiwango cha C+, hoja moja au mbili asipite kiwango cha C-
ii. Hoja zote zijadiliwe kikamilifu.
iii. Aweze kuwa na idadi sawa ya hoja katika pande zote. almuradi aonyeshe msimamo wake. Asipofanya hivyo asiadhibiwe lakini asipite kiwango cha B.
iv. Akishughulikia upande mmoja tu bila kugusia upande wa pili asipite asipite kiwango cha C+.

3. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
-Kisa kidhihirishe hali ya kufanya au kurekebisha jambo mapema.
-Unapokosa kufanya hivyo utapata matatizo mengi baadaye au ikubidi ufanye jambo kubwa sana kuliko lili la awali.
-Atunge kisa kimoja tu, na wala sio visa.
-Kisa kiwe na urefu ufaao na kioane na methali.
-Kisa kisichooana na methali, apate 03.
-Akiegemea upande mmoja tu wa methali, asipite kiwango cha C+.

4. Kisa cha mwanafunzi kimalizikie kwa maneno ya madokezo aliyopewa.
-Atakayeanza na maneno ya madokezo, atakuwa amepotoka. Kwa hivyo apewe kiwango cha D.
-Asipomalizia kwa mdokezo aliopewa na kisa chake kihusiane na mdokezo, atakuwa hajapotoka kimaudhui bali amepungukiwa kimtindo.
-Atakuwa amepotoka kimaudhui pale tu atakosa kumaliza kwa kauli aliyopewa na kusimulia kisa kisichohusiana na swali.
-Ajihusishe na kisa (atumie nafsi ya kwanza) Asiyejihusisha amelemewa kimtindo.

<u>Tanbihi</u>: Mwalimu atumie mwongozo wa kudumu kwa maelezo zaidi kuhusu utahini katika viwango mbalimbali.